# *KUSHINDANA KI HALALI*

"Hata mtu akishindana katika *michezo hapewi taji, asiposhindana kwa halali"* (2Timotheo2:5)

*"Je! Hamjui, yakuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate. Na kila ashindae katika mchezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo, kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isio haribika".* (1korintho 9:24-25)

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alichosema kuhusu hilo:

Na kila mmoja wenu anajua hilo katika michezo ya olimpiki au michezo yoyote ya riadha, haijalishi kama umefika wa kwanza katika mashindano, lakini kama hukucheza mchezo kwa sheria\kanuni zake, unakataliwa. Inabidi ucheze kwa sheria \kanuni sawa. Na hivyo ndivyo ilivyo katika maisha ya kibinadamu. Huwezi ukacheza isivyosahili kinyume na sheria za mchezo wa maisha, na utegemee kushinda. Inabidi ucheze hiyo sawasawa na Neno la Mungu. Na kwa kusudi ambalo limekuweka hapa. [1]

Haijalishi aliyekuwa wa kwanza kufika ni nani, lazima ucheze sawa na kanuni za mchezo sivyo hutaweza kushinda kamwe. Kama mkimbiaji anakimbia kwa kuzunguka njia, na mwingine akachukuwa njia ya kukatiza mkato, na kumshinda yule aliyezunguka kwa kiasi cha nusu saa, bado atakaliwa mwishoni mwa mashindano. Lazima acheze sawa na kanuni za mchezo sivyo atakataliwa.

Na hivyo ndivyo tupaswavyo kufanya, katika mashindano tukimbiayo ya maisha sasa, lazima tucheze sawa na kanuni za Mungu au sivyo tutakataliwa tukifika pale. Hata kama ni raisi, au sisi ni magavana, au wahuduma au ni watu wa kanisa fulani, au dhehebu fulani, kanuni za mchezo ni lazima zifuatwe. Lazima tucheze kihalali; lazima tucheze kwa kutumia taratibu. Lazima tuhubiri Neno, tufanye hivyo kwa kupenda.

Paulo alisema katika waebrania12:1 "Basi na sisi pia kwakuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, na



tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyokuwa mbele yetu," Paulo alikuwa anazungumzia olimpiki na kadhalika, ambayo ilikuwa kule Ugiriki na Roma, na kadhalika; alijua ya kuwa unapaswa kucheza ule mchezo kihalali, kwa maana kama hukufanya hivyo, unakataliwa.

Na leo, kama wakristo waliozaliwa mara ya pili, kama waaminio hapa wa wakati wa mwisho, inabidi tuucheze mchezo sawasawa na kanuni zake. Inabidi tupige mbio kwa saburi katika mashindano yaliyowekwa mbele yetu; Tukimwangalia mwanzilishi na mkamilishaji Yesu kristo (waebrania12:2) [2]

Halafu ninaambiwa kwamba, Napolioni, yule mshindi wa siku zilizopita, miaka kadhaa, kama mitano, nilipata heshima ya kusimama karibu na Wateroo. Nanikachukuwa kakitabu kadogo pale, (pale uwanja wa ndege) na nilikuwa ninasoma maisha ya Napolioni. Aliwachukuwa Wafaransa. Nae akaja ufaransa, akawa amezaliwa katika kisiwa na akaja Ufaransa ili kuwakomoa, lakini akawa mshindi mkuu. Alikuwa mtu mtaratibu kwa kuanzia, lakini mafanikio yakamlewesha. Na inasemekana, "kwamba wanawake, walipoteza watoto wao vitani, kwamba aliogopewa (Aliuwa kila kitu ambacho hakikubaliani naye) kiasi kwamba wanawake badala ya kusema, "lile jitu zimwi litakuchukuwa! Wangesema, "Napolioni atakuchukuwa". Na kijani mdogo mwenye macho maangavu wataficha vichwa vyao haraka, wakilifikiria hilo jitu katili Napolioni.

Lakini unaona ule ushindi alioshinda, haukudumu.

Alikuwa ni mpiga marufuku wa vitu kwa kuwazia, na alikufa akiwa na umri wa miaka thelathini na tatu mlevi. Ushindi wa namna hiyo haudumu, kwasababu hauletwi kwa namna iliyo sahihi. Huwezi kupata kizuri kutoka kibaya, Lazima ucheze mchezo kwa kanuni halali ziridhishazo [1]

Lakini alishindwa, kwa sababu kamwe hakucheza kwa usahihi kanuni za mchezo. Na kumbuka hili tu; kwamba, hilo ni fundisho zuri kwa kanisa la Mungu aliye hai.

Kama hatuchezi mchezo kwa kanuni zake, tutakataliwa kule mwisho, lazima kushika kanuni za mchezo ili kushinda.

Na kama kanuni za mchezo mahali hapa, ni lazima mtu azaliwe mara ya pili ili aingie kwenye ushirika na Kristo na kanisa lake (Yohana3:1-8), na tunaweza kuwa dhehebu kubwa duniani, lakini kama

hatukucheza kanuni za mchezo kwa usahihi, tutakataliwa kule mwisho. Lazima tuje moja kwa moja na kanuni za Mungu. Sio kanuni zetu; ambazo inapasa tuzishike. Tunapiga mbio sawa na kanuni zake, na inibidi tuzishike hizo (Yohana15:7)

Kwa hiyo unaona, Napolioni, baada ya kuwa shujaa mkubwa, na mshindi mkuu, aliwashinda watu kwa kuwatia hofu, na hiyo siyo kanuni ya mchezo. Kanuni ya mchezo ni kushinda kwa Upendo.

Hakuna nguvu nyingine katika dunia yote iliyo kuu zaidi ya Upendo (1korintho13:1-3) Nami ninaona kwa sehemu kubwa kwetu, tumeweka mchezo juu ya kanuni nyingine ambazo(simaanishi kuwa mkali lakini wakati mwingine), tumezitengeneza wenyewe, na kuweka mkazo mkubwa katika kanuni hizo, na kujikuta tu wenyewe tukikataliwa. [3]

Lakini uone, kama mtu nimshindi, ni lazima makusudi yake yawe sahihi na Malengo yake yawe sahihi.

Na kama huchezi mchezo kihalali, ni hakika utashindwa/utapoteza, haijalishi wewe ni mshindi kiasi gani. Lazima ufuate kanuni za mchezo ili uwe mshindi. Na kama unadanganya, utatolewa kwenye mchezo, haijalishi ni mchezaji mzuri namna gani.

Vipi kama Martini Luther angecheza kanuni za mchezo, kwa usahihi? Kusingekuwa na kanisa la Methodist.

Vipi kama wamethodist wangecheza kanuni za mchezo sahihi? Kusingekuwa na kanisa la kipentekoste.

Lakini kama tunashindwa kucheza kanuni za mchezo kwa usahihi, Mungu atatukataa sisi na kuinua uzao wa lbrahimu kutoka kwenye mawe haya.

Na Mungu anataka mchezo uchezwe kisahihi, na nilazima tufanye hivyo. Kwa hiyo haijalishi tunajisikia tunaendelea vipi, hiyo haifanyi tofauti, mpaka tuje kwenye kanuni za mchezo………..

"kama Mungu amekupa kipawa, kaa na hicho kipawa hakifanyiwi kazi, haijalishi ni kikubwa kiasi gani, kama hakikufanyiwa kazi sawa na kanuni, bado utakataliwa katika shindano".

Na nguvu kuu sana ni ijuayo ni Upendo(ileishara). "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na malaika, kama sina upendo sikitu mimi au nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapo kuwa na nguvu kiasi cha kuhamisha milima, kama sina Upendo sikitu mimi"(1korntho13:1-33! (Galatia5:13-15).



Kama tutaemda kushinda, lazima tuje kwenye kanuni za kushinda. Ishara na maajabu hizi zote kuu, ambazo tunapona tunampa Mungu sifa. Lakini kama mambo haya hayakujegwa juu ya upendo wa Mungu wa kikristo na heshima kwa Mungu wa watu wake, vitashindwa(warumi12:9-21). Lazima vitashindwa. Unaona? Kwasababu havina msingi.[4].

Kama unae mtu mgonjwa amelala hapa, au mwenye dhambi amelala hapa au mtu anaetaka kuwa sahihi (hawezi kushinda ulevi, hawezi kuacha kuvuta sigara, hawezi akaacha tamaa na mengineo)! Kama tu utatenda kwa sheria za Mungu, kumuacha Roho mtakatifu aje pale, hapo sasa sio yeye mwenyewe tena. Ataacha jambo hilo,kwa sababu Roho mtakatifu anamshindia\anamwinua juu ya hilo. Lakini lazima utende sawa na sheria za Mungu, kanuni za Mungu. Tubu na ubatizwe……(matendo2:38-39) [5]

Mungu hana kibadala, hakuna ila damu. Hana njia za mkato au vichochoroni. Lazima uje katika njia ya Mungu kupitia upatanisho kwa damu (wakolosai1:19-2, 2korintho5:17-79) na hapo unakuwa mwana na binti wa Mungu (yohana1: 12-13). Halafu mambo yote yanawezekana. Hapo miujiza inawezekana, uamsho/ ufufuo unawezekana. [6]

Watu leo wanataka njia za mkato. Wako nje huku leo na wanaendelea (oh jamani), na kesho wanatoka kuhubiria watu pentecoste wanawaacha wafanye hivyo pia. (1timotheo3:1-6). Ndio wanataka njia za mkato kwenda mbinguni," Halleluya, yote nipaswayo nikwenda pale chini na nisifikirie chochote kabisa, na niseme, Halleluya, halleluya, Ninalo vazi la Eliya nimelivaa, kesho nitaenda nje kutoa mapepo. Halleluya, halleluya, nimelipata Mungu nasifiwe, ninakwenda". Wanataka njia ya mkato ya mbinguni, wakichukuwa ulimwengu kadri wawezavyo. Huwezi kuchukua chochote cha ulimwengu. Hakuna njia za mkato unakuja kupita kalvari. Unakuja kwa njia ya madhabahu ya shaba. Unakuja kwa njia ya nyoka wa shaba. Unakufa unakufa hasa, unakufa, unakufa kihalisi kabisa katika utu wako, unakufa kwa mambo ya dunia na unazaliwa upya yohana12:24-25, 1yohana5:6-8) Amen. Hakuna dunia, mambo ya dunia yamekufa (wagalati2:19-20)

Hakuna njia za mkato. Unaona? Wanataka waje tu kwa haraka; hawataki kukuwa. Tunakuwa katika Bwana. Inachukuwa kukuwa na uzoefu (2korntho3:18; Efeso2:21-22) Hii "kuwa tajiri kwa usiku mmoja". Nilikuwa na rafiki yangu wakati mmoja ambaye alikuwa anaweka akiba ya maisha yake katika benki, na anachukuwa faida kidogo, na mmoja akaja na njia ya mkato. Unajua, tunasikia mengi leo, njia za kurahisisha. Dunia imejaa hayo matangazo, na televisheni, redio, magazeti. Na kama watu wa Amerka wanaangukia hayo!
Nami nasema hili kwa heshima na kicho, na ninaamini ni halisi ni kama mzaha, lakini jambo hili limeingia katika mwenendo wa kanisa. Mungu hana njia za mkato. Unapaswa ulime ile gharama (waebrania12:14-17). Unakuja na uchukuwe njia Mungu alio itengeneza kwa ajili yetu (matayo7:13-14; matayo16:24-26) [8]

Dunia na watu wanaangalia kimwanya kidogo, kanjia kadogo njia ndogo za mkato, lakini hakuna njia za mkato kwenye neno la Mungu. Kuna namna mmoja tu ya kimfano. Lazima ujikane mwenyewe(kolosai2:11-12) na ulingane na hicho kimfano. Sio ujaribu kutaka hicho kimfano kilingane nawe. Kila mmoja lazima afanye hivyo. Hiyo ndio njia pekee Mungu alionayo ya kulitenda hilo [9].
Nukuu za kingereza;

[1] Imani Ndio Ushindi Wetu(58-1004)Aya6-7
[2] Kile Kinachohitajika Kushanda Kutokuamini Kote(60-0729)Aya E-Siff
[3] Mshindaji Mkuu (58-0610), Aya E-6-E-7
[4] Mshindaji Mkuu (58-01100),Aya E-7-E-10
[5] Kwanini Tumepewa Roho Mtakatifu(59-1217) Aya 45
[6] Upatanisho Kupitia Ushirika(56-0120) Aya E-38
[7] Lazima Uzaliwe Mara Ya Pili(61-1231m),Aya 140-146
[8] Kuwekeza(63-1116b),Aya 44/48
[9] Manukato Huwekwa Wazi Na Unabii(65-0801), Aya51.

*jiwe la kiroho la kujengea na 172 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*